JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO

SHULE YA SEKONDARI CHIGELA
S.L.P. 40 GAIRO-MOROGORO.

**Namba za Simu**

**Mkuu wa shule: 0715144744**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0653222013**

**Mwalimu wa taaluma: 0688694222**

**Mwalimu wa nidhamu: 0759554028**

**Patron: 0680330059**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**……………………………………………………………………….**
**S.L.P …………………………………………………………….**
**……………………………………………………………………….**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHIGELA HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO MKOA MOROGORO MWAKA …………..**

## 1.0 UTANGULIZI.

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya sekondari Chigela mwaka ……… na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Chigela ipo umbali wa Kilometa 3 kutokea stendi ya Gairo jirani na barabara kuu inayoelekea Morogoro kutokea stendi ya Gairo. Usafiri

kutoka stendi ya Gairo unapatikana ,Nauli ni Shilingi 3000/- kwa pikipiki na Shilingi 1000/- kwa gari la abiria.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ……………… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………………

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare za Shule.

i) **Wakati wa Darasani(Muda wa Vipindi);**

- ✓ Suruali rangi ya Dark Blue Stimu (Grade I) mbili (02) pana (Taniapu Inch 15 hadi 16), marinda manne madogo mbele (kushoto mawili na kulia mawili), mifuko yake (miwili ya mbele ya kawaida kushoto mmoja na kulia mmoja na nyuma mmoja upande wa kulia).
- ✓ Shati mbili (02) nyeupe za tetron mikono mirefu aina ya tomato yenye mfuko mmoja yasiyobana.
- ✓ Soksi nyeusi saizi ya kati pair 3 zisizo na pambo lolote
- ✓ Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba viwe na kisigino kifupi.
- ✓ Sweta rangi ya Dark Blue.
- ✓ Tai 2 rangi ya dark blue zenye mistari myeupe, zitapatikana shuleni kwa Tsh 5,000 kila moja.
- ✓ T-shirt ya shule rangi ya kijivu (grey) inapatikana shuleni kwa Tsh 12,000 na inavaliwa siku za jumatano na ijumaa.

**ii) Baada ya muda wa Darasani(Vipindi kuisha/Shamba Dress);**

- ✓ Suruali rangi ya Damu ya Mzee (Redish Brown) mbili (02) pana (Taniapu Inch 15 hadi 16), marinda manne madogo mbele (kushoto mawili na kulia mawili), mifuko yake (miwili ya mbele ya kawaida kushoto mmoja na kulia mmoja na nyuma mmoja upande wa kulia).
- ✓ T-shirts mbili (02) za njano maarufu kama form six isiyo na maandishi yoyote za kushindia.(shamba dress).
- ✓ Raba nyeupe na Viatu vyeusi aina ya Clarks (Clarks shoes) pair moja.

**iii) Sare za Michezo ni:-**

- ✓ T-shirt rangi ya blue plain , Kaptura au Bukta rangi ya blue plain (Jezi).
- ✓ Track suit rangi nyeusi.
- ✓ Soksi za michezo rangi nyeusi.
- ✓ Raba/viatu vya michezo.

**iv) Sare zingine zinazoruhusiwa kuvaliwa shuleni ni pamoja na;-**

- ✓ Fulana nyeupe za ndani mbili au zaidi(Vesti).
- ✓ Nguo za ndani (boxers) kuanzia 3 na zaidi.
- ✓ Leso (handkerchief)
- ✓ Viatu vya wazi vya kuogea(Ndala)
- ✓ Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali

## 2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 12 (*counterbook Quire 3*);
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Kalamu za wino za kutosha
iv. Penseli, Kifutio,pamoja na rula
v. Mathgematical set
vi. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);
vii. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni futi mbili na nusu (2.5)
viii. Mashuka Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*shuka light blue na foronya zake);*
ix. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
x. Scientific Calculator
xi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xiii. Kwanja 1, jembe 1 na mpini wake, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje na mopper 1.
xiv. Graph pad 02 Kwa kila mwanafunzi

xv. Taa ya sola- Kwa ajili ya matumizi ya kujisomea umeme unapokatika
xvi. Disposable gloves 1 box Kwa wanaosoma CBG
xvii. Laboratory coat Kwa wanaosoma CBG
xviii. Bima ya afya
xix. Faili moja kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za taarifa zake shuleni pia yanapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 3000/=.
xx. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
xxi. Hati ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne (result slip)
xxii. Pocket money.

## 2.3 Michango mbalimbali

**Michango ifuatayo ilipwe kwenye akaunti ya shule, CRDB A/C NA. 0150865351700 (CHIGELA SECONDARY SCHOOL).Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye Pay in slip ya bank.**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 2.4 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**2.5 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**Mkuu wa Shule: 0715144744**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0653222013**

**Mwalimu wa taaluma: 0688694222**

**Mwalimu wa nidhamu: 0759554028**

**Mwalimu wa fedha: 063953881**

**Patron: 0680330059**

### 2.6 Sheria za Madarasani

✓ Ukiukaji wa sheria hizi utasababisha mwanafunzi kupewa adhabu kali:-

- **i.** kelele za aina yoyote haziruhusiwi darasani. Kumbuka darasani ni mahali pa kujifunzia, sio pa kupiga kelele.
- **ii.** Ni lazima kila mwanafunzi akae darasani kwa kufuata mpango uliowekwa, kutofanya hivyo ni kukiuka sheria.
- **iii.** Hakuna mwanafunzi atakayetoka nje ya darasa wakati wa vipindi bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa.
- **iv.** Ni marufuku kuingia na chakula/kinywaji darasani au kula darasani.
- **v.** Ni marufuku mwanafunzi yeyote kuandika maandishi yoyote kwenye dawati, kiti, meza, sakafu, kuta au paa za darasa/ofisi Adhabu kali itatolewa kwa atakayebainika kufanya hivyo.

**"Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi na nadhifu muda wote awapo shuleni, avae sare ya shule inavyo stahili na ni marufuku kuvaa mlegezo."**

### 3.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa na mwanafunzi shuleni ni pamoja na;

(a) **Medical Examination Form**,
Hii ni fomu ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule utapokua unarepoti shuleni.

(b) **Fomu ya maelezo binafsi ya kuhusu historia ya mwanafunzi/Mkataba**

Hii ni fomu maalumu ya maelezo ambayo itasimulia historia ya mwanafunzi kwa ufupi hasa vipengele muhimu vinavyohitaji uangalizi wa karibu na kuahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Fomu hii pia pia utaikabidhi ofisini kwa mkuu wa shule utakapo ripoti.

(c) **Tamko la mzazi /mlezi kukiri kukubaliana na sheria za shule**
Fomu hii ni tamko maalumu la mzazi kuahidi kushirikiana na shule katika kumuwezesha mwanafunzi kusoma bila vikwazo.

(d) **Fomu ya Taarifa binafsi za Mzazi/Mlezi kuhusu Mwanafunzi,**
Hii ni fomu maalumu kwa ajili ya taarifa za usajili wa Mwanafunzi shuleni. Hivyo ijazwe kikamilifu na kwa usahihi mkubwa.(ijazwe na mzazi)

**Tafadhali soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kujadiliana na mwanao juu ya utayari wake katika kuzingatia yaliyo tajwa kwenye fomu hii na kuyatekelezakikamilifu**

*karibu sana shule ya sekondari Chigela*

EDSON MFAUME MARTIN
MKUU WA SHULE

*"Eduacation is our prosperity"*

## CHIGELA SECONDARY SCHOOL

## A- LEVEL SUGGESTION BOOKS REQUIREMENT

**GEOGRAPHY BOOKS**

(1) Waugh D (2009) Geography an Intergraded Approach, Nelson Thomas Uk

(2) Leongh C.G and Morgan C. Gillian (1972) Human and Economic Geography Second Edition Oxford

(3) Bunnett R.B(1973) General Geography In Diagram Longman

(4) Pritchard J.M And Munowenyu E(1988) A Certificate Geography Of Zimbabwe Longman Zimbabwe Ltd

(5) Ahmed Rubwama (2013) Elementary Physical Geography

(6) Daniel Sagatha (2014) Practical Geography For East Africa

**(7)** Pritchard J.M Practical Geography

**HISTORY BOOKS**

1. Contemporary Historical Events (Paper 1 And Paper 2) By Mwalimu Shibitali Ck Tumaini
2. Essentials In Advance Level History (Paper 1 And Paper 2) By Saleh Yassin
3. Mastering Advanced Level History (Paper 1 And Paper 2) By Mwalimu Kato Abubaker Kassim

**CHEMISTRY BOOKS**

1. General Chemistry By Tanzania Institute Of Education(Tie)
2. Physical Chemistry By Tanzania Institute Of Education(Tie)
3. Organic Chemistry By Tanzania Institute Of Education(Tie)
4. Inorganic Chemistry By Tanzania Institute Of Education(Tie)
5. Ngaiza,A Level Chemistry Series
6. Unga ,A Level Chemistry Series
7. A Level Chemistry Practical By R.S. Mlungu

**BIOLOGY BOOKS**

1. Biology Student Book Form FiveBy Tanzania Institute Of Education(Tie)
2. Biology Student Book Form Six By Tanzania Institute Of Education(Tie)
3. Complete Advanced Biology Form Five By Respicius Rwehumbiza
4. Complete Advanced Biology Form Five By Respicius Rwehumbiza
5. Understanding Biology

6. Biological Science(Bs)

**KISWAHILI.**

1. Nadharia ya Lugha Kiswahili 1, Kidato cha 5&6.
2. Sarufi na Fasihi – Sekondari na Vyuo. Dar –es- Salaam, Tanzania Publishing House- Nkwera F. 1987
3. Fasihi ya Kiswahili – Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Mulokozi M. 1996.
4. Ushairi: Nadharia na Tahakiki Dar – DUP, Senkoro F. 1988.
5. Kiswahili Sekondari Kidato cha Tano – T.E.T – 2016.
6. Kamusi ya Kiswahili Sanifu.
7. Sarufi miundo ya kiswahili sanifu- SAMIKISA.
8. Sarufi maumbo ya kiswahili sanifu – SAMIKISA.

**RIWAYA.**

9. Mfadhili.............................Hussein Tuwa
10. Kufikirika.........................Shaban Robert
11. Vuta N'kuvute---------Shafi Adam Shafi
12. Usiku utakapokwisha.—Mbunda Msokile

**TAMTHILIYA.**

13. Kivuli kinaishi................Ibrahim Hussein
14. Nguzo Mama................Emmanuel Mbogo
15. Morani.......................Said Mohamed
16. Kwenye ukingo wa Thimu........Ibrahimu Hussein

**USHAIRI.**

17. Kimbunga...................Haji G.Haji
18. Chungu Tamu............Theobald Mvungi
19. Fungate ya uhuru...........Mohamed S.Khatibu
20. Mapenzi Bora

**ECONOMICS**

21. Economics 1 and 2 TIE BOOKS
22. Simplified economics
23. Micro economics student’s book
24. Macro economics student’s book
25. Ambilikile one
26. Ambilikile two
27. Principle of economics

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI YA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**

- ✓ **TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI:**
  - xii. JINA LA MWANAFUNZI ___________________________________
  - xiii. TAREHE YA KUZALIWA______________
  - xiv. MAHALI ULIPOZALIWA (MKOA NA WILAYA) ___________
  - xv. MAHALI UNAPOISHI ________________________________________
  - xvi. URAIA ______________
  - xvii. SHULE ULIYOTOKA ____________________________________
  - xviii. NAMBA YA MTIHANI (CSEE) _______________

- ✓ **TAARIFA YA MZAZI AU MLEZI:**
  - ✓ JINA LA MZAZI/ MLEZI________________________________________
  - ✓ KAZI YA MZAZI/ MLEZI _____________________________________________
  - ✓ ANUANI YA MZAZI/ MLEZI _____________________________________________
  - ✓ NAMBA YA SIMU YA MZAZI/ MLEZI ____________________________________________

  JINA NA NAMBA YA SIMU YA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

  (ii) JINA_______________________
  NAMBA YA SIMU______________

  (iii) JINA______________________
  NAMBA YA SIMU______________

  - BARUA PEPE (EMAIL ADRESS) YA MZAZI/ MLEZI KAMA IPO______________________________

- ✓ **KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA**:

Mimi__________________________.Kidato cha________Mwaka_______Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote, nakubali kuipokea / sikubali kuipokea nafasi niliyopewa,nathibitisha kwamba nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa. Naahidi kuyazingatia.
Tarehe__________________________Saini_________________

**D.KUKUBALI SHERIA ZA SHULE**

**MWANAFUNZI**

Mimi________________________________nimezisoma nakuzielewa sheria na ninaahidi kwamba nitazingatia sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu na viongozi wote wa shule,nikikiuka sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni,taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe ________________Saini _______________

**E. MZAZI (AJAZE SEHEMU HII)**

**MZAZI**

- ✓ Mimi mzazi/mlezi wa ____________________________ nimeleewa maagizo na ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanangu ni __________________________ na dhehebu yake ni ________________________.
- ✓ Ninaruhusu mwanangu kushiriki katika makongamano au warsha za kidini nje ya shule hususani zile zinazofanyika nje ya mkoa wa Morogoro anapokuwepo na mwalimu mlezi wa shule hii.
- ✓ Ninaruhusu likizo fupi atoke shuleni na kwenda kwa ___________________________________

  Uhusiano wake na mwanangu ni _____________________ namba yake ya simu ______________________.
- ✓ Aidha,mimi _______________________________________ ambaye ni mzazi nimesoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi _______________________________________ na ninaahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa mzazi /mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kutimiza mahitaji yake ya shule.

_______________________________ _______________

**JINA LA MZAZI/MLEZI** **SAINI YA MZAZI**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**Student name ___________________________**
**Date ___________________________________**
**Signature _______________________________**

**PART A:**

**From The Headmaster,**
**Chigela Secondary School,**
**P.O.Box 40,**
**GAIRO**

## TO THE MEDICAL OFFICER

**Please examine the above-named student as to her physical and mental fitness for a full-time student. The examination should include the following category (a-d)**

a) **(i) Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Limbs (v) Venereal diseases (vi) Leprosy (vii) Epilepsy**
b) **Neurosis**
c) **Other serious diseases e.g. Asthma, T.B etc.**
d) **Pregnancy**

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

**(To be completed by Government Medical Officers) I have examined the above-named student and consider that he is fit/unfit for full time studies.**

i. **Eyesight_______________________________________________**
______________________________
ii. **Hearing_______________________________________________**
_____________________________
iii. **Speech**
_______________________________________________________
_______________________
iv. **Limbs**
_______________________________________________________
_______________________

v. **Venereal diseases______________________________________________**

**____________________**

vi. **Leprosy________________________________________________**

**_________________________**

vii. **Epilepsy_______________________________________________**

**________________________**

viii. **Neurosis**

**________________________________________________________**

**____________________**

ix. **Other serious diseases**

2) **Asthma_________________________________________________**

**_____________________**

3) **T.B**

**________________________________________________________**

**____________________**

x. **Pregnancy______________________________________________**

**_________________________**

**Other comments:**

**________________________________________________________**

**________________________________________________________**

**________________________________________________________**

**Name ________________________________ Date _____________________**

**Signature ____________________**

**STATION _________________________________________________**

**DESIGNATION ______________________**

**N.B. I request this form to be returned to the school in a sealed envelope.**